## APRM ni nini?

APRM ni mojawapo ya Taasisi za Umoja wa Afrika. APRM ni kifupi cha **African Peer Review Mechanism** - Mpango wa Hiari wa Nchi za Umoja wa Afrika Kujipima kwa Vigezo vya Utawala Bora. Mpango huu ulibuniwa na viongozi wa Umoja wa Afrika mwaka 2003 ili kuziwezesha nchi wanachama kujitathmini kwa vigezo vya utawala bora katika maeneo makuu manne ambayo ni:

- Demokrasia na Utawala wa Kisiasa;
- Usimamizi wa Uchumi;
- Utendaji wa Mashirika ya Biashara na;
- Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi

Kimsingi kuanzishwa kwa APRM ilikuwa ni sehemu ya kutekeleza malengo ya iliyokuwa Mpango Mpya wa Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika (NEPAD), kwa dhana kuwa maendeleo thabiti ya kiuchumi Barani Afrika yanategemea kuwepo kwa utawala bora katika siasa, uchumi na huduma muhimu za kijamii.

## Malengo ya Mpango

Lengo la msingi la APRM ni: Kuhimiza utekelezaji wa sera, viwango na mienendo inayokubalika kitaalamu ili kujenga utengamano wa kisiasa; Ukuaji chanya wa uchumi, maendeleo endelevu na kuharakisha ushirikiano wa kiuchumi wa Kikanda na hatimaye kwa Bara zima la Afrika; Kubadilishana uzoefu na kuimarisha mafanikio yanayopatikana, na pia kutambua changamoto zilizopo na kushirikiana kuzigeuza kuwa fursa za maendeleo.

## Muktadha wa APRM Tanzania

Tanzania iliweka saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa kujiunga na Mpango wa APRM mnamo 26 Juni, 2004, Bunge la Jamhuri ya Muungano likaidhinisha Mpango wa APRM kupitia Azimio Na. 18 la tarehe Februari 1, 2005. Wizara ya Mambo na Nje Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliteuliwa kuwa Wizara unganishi kati ya Serikali, APRM Tanzania na Makao Makuu ya APRM yaliyoko Afrika ya Kusini. Pia liliundwa Baraza



*Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Muungano akishuhudia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete; Rais wa Awamu ya Nne akisalimiana na Dr Salim S Nasser, Mjumbe wa Baraza la Taifa APRM Tanzania kutoka Zanzibar, katika dhifa iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam, Machi 2012.*

la Usimamizi la Taifa lenye wajumbe kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Sekta Binafsi, Vyama vya Wafanyakazi na Asasi za Kiraia.

## Mchakato wa APRM

Mchakato wa APRM hushirikisha makundi mbalimbali katika kueleza changamoto za kiutawala zinazowakabili. Mchakato wa APRM hasa unahusu tathmini ya Utawala Bora inayofanywa na Wataalamu wa ndani ya nchi na ule unaofanywa na Wataalamu toka nje ya nchi. Mchakato huu hupitia hatua muhimu zifuatazo:

**Hatua ya Kwanza:**

- Mchakato wa ndani ya nchi unahusu utafiti wa Maktaba unaolenga kupata takwimu na maelezo mengine juu ya hali halisi ya uatwala bora. Pia, maoni ya wananchi wa kawaida, na maoni ya wataalamu hukusanywa kwa kutumia hojaji ya kaya na hojaji ya wataalamu.
- Utafiti wa Maktaba na maoni yaliyokusanywa huunganishwa pamoja ili kupata Ripoti ya Nchi juu ya Utawala Bora. Kisha Mpango Kazi wa namna ya kutatua changamoto zilizobainishwa hutayarishwa. Ripoti ya ndani ya nchi na Mpango Kazi huwasilishwa katika Sekretariati ya APRM ya Bara Afrika iliyopo nchini Afrika ya Kusini.

**Hatua ya Pili:** Hatua inayofuatia ni kufanyika kwa tathmini ya Utawala Bora na wataalamu kutoka nje ya nchi. Wataalam hawa hutembelea nchi husika na kukutana na wadau mbalimbali na kupata maoni yao juu ya utawala bora katika nchi yao. Baadae, wataalamu hao hutayarisha Ripoti ya Nchi juu ya Utawala Bora na Mpango Kazi na namna ya kutatua changamoto zilizobainishwa. Serikali ya nchi husika hupata fursa ya kujibu hoja zilizopo kwenye Ripoti.

**Hatua ya Tatu:** Hatimaye, Ripoti na Nchi, Mpango Kazi pamoja na Majibu ya Serikali yakiwa yameambatanishwa kwenye Ripoti huwasilishwa mbele ya Kikao cha Wakuu wa Nchi wanao shiriki katika mchakato wa APRM na kujadiliwa.

**Hatua ya Nne:** Miezi sita (6) baadae, Ripoti hiyo huwa tayari kusambazwa kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Bunge la Afrika, Taasisi za Kikanda, wananchi n.k.

**Hatua ya Tano:** Utekelezaji wa Mpango Kazi unaohusu Ripoti ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM) Tanzania ya mwaka 2013 ikiwa ni pamoja na kujibu hoja mbalimbali zilizomo kwenye Ripoti husika zinazojielekeza zaidi katika kipindi cha miaka ya 2013 hadi 2019 ambapo takwimu za uhakika zimekwisha chapishwa.

## Mchakato Ulivyofanyika Tanzania

Mwaka 2007, taasisi nne (4) ziliteuliwa baada ya kufanyika ushindani wa wazi ili kufanya utafiti chini ya APRM. Taasisi hizo ni:

| | |
|---|---|
| **Idara ya Siasa** | Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (Utawala Bora katika Siasa na Demokrasia |
| **Idara ya Uchumi** | Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (Usimamizi wa Uchumi) |
| **Kitivo cha Sanaa** | Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (Utendaji wa Mashirika ya Biashara) |
| **Taasisi ya Kupunguza Umaskini (REPOA),** | Dar Es Salaam (Maendeleo ya Jamii) |

Baada ya Taasisi hizo kuandaa Ripoti zao. Wataalamu wengine walizipitia ili kuhakiki na kushauri juu ya ubora wake. Ripoti hizo ziliunganishwa na kuwa Ripoti moja ya nchi. Mpango Kazi uliandaliwa kwa kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali za uchumi. Ripoti ya Ndani ya Nchi ilikuwa tayari mwaka 2009, Sekretariati ya APRM Tanzania kwa kushirikiana na Baraza la Usimamizi la Taifa liliandaa semina ya kuwafikia kwa mara nyingine wananchi na wadau mbalimbali ili kuihakiki na kuiboresha Ripoti hiyo. Wataalamu kutoka nje ya nchi waliitembelea Tanzania Machi 21 2012 na kuandaa Ripoti ya Nchi. Tanzania iliwasilisha Ripoti hiyo kwenye Kikao cha Wakuu wa Nchi wanaoshiriki Mpango wa APRM mnamo Januari 2013. Baada ya uwasilishaji wa Ripoti, Mpango Kazi wa mapendekezo ya kutatua changamoto zilizobainishwa kwenye Ripoti uliendelea kutekelezwa kutoka mwaka 2014 – 2019. Kwa sasa, Rasimu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM Tanzania imekwishaandaliwa na inaendelea kufanyiwa uhakiki na wadau.

## Manufaa ya Mchakato

- Taarifa za APRM ikiwa ni pamoja na taarifa ya Ndani na taarifa ya Nchi zimekuwa rejea muhimu katika masuala ya utawala bora nchini;
- Mpango wa APRM umesaidia katika kuongeza kada ya Wanataaluma wa masuala ya utawala bora nchini ambao watatumika kitaifa na kimataifa;
- Jamii imefahamu yaliyomo kwenye taarifa ya Ndani, taarifa ya Nchi na kufuatilia utekelezaji wa Mpango Kazi wa kutatua changamoto za Utawala;
- Jamii imekuwa na uelewa kuhusu mchakato wa APRM wa Kujipima katika utawala bora, faida zake na umuhimu wa kushiriki katika tathmini za utawala bora;
- Kutokana na kuwa na mfumo bora wa tathmini na ufuatiliaji kumekuwa na ufanisi wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM;
- Baadhi ya Wizara, Idara na Wakala za Serikali zimefanikiwa kutenga fedha katika Mipango yao ya Muda wa Kati kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi changamoto za utawala bora na kuandaa taarifa za utekelezaji;
- Wabia wa Maendeleo na Wawekezaji wamepata taarifa ya hali halisi ya utawala bora nchini kupitia taarifa mbalimbali zinazotolewa na APRM;

## Uhamasishaji wa APRM Tanzania

Mchakato huu wa APRM nchini Tanzania ulianza kwa kufanya uhamasishaji kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mikutano ya hadhara nchi nzima. Makundi mbalimbali yalifikiwa ambapo kati yao ni: Makatibu Wakuu wa Wizara Tanzania Bara na Zanzibar; Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Baraza za Wawakilishi – Zanzibar; Waandishi wa habari; Asasi za Kiraia; Vyama vya Ushirika; Vyama vya Siasa; Taasisi za Elimu ya Juu; Viongozi wa vikundi vya Wanawake; Vijana na Madhehebu ya dini. Wengine ni Makatibu Tawala wa Mikoa; Wakurugenzi wa Majiji; Manispaa; Miji na Wilaya; Jukwaa la Wahariri; Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa; na maofisa wengine wa Serikali na wananchi wa kada nyingine za kawaida.

## Mawasiliano na Wadau

Mkakati wa sasa ni kuongeza nguvu katika kuimarisha zaidi mawasiliano ya umma kati ya APRM Tanzania na wadau wake ili kuwajulisha taarifa za mara kwa mara kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano ya umma ambazo zinaweza kuwafikia Watanzania wengi zaidi na kwa haraka, kwani huu Mpango ni wa kila mmoja wetu, unaogusa maisha yetu. Hivyo basi, ni jukumu la kila Mtanzania kujua tathmini ilivyoendeshwa, mchakato umebaini nini, na pia kwa vipi mwananchi atafaidika na fursa za kimaendeleo zitokanazo na mabadiliko ya maoni aliyoyatoa hapo awali.

## Malengo ya Baadae

Mchakato wa APRM pindi unapokamilika, shughuli za Sekretariati ya kila nchi mwanachama ni kuendelea na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi na kuhakikisha yale mazuri yaliyoainishwa kwenye Ripoti yanaendelezwa na huku zile changamoto zilizoainishwa nazo zinafanyiwa kazi.

Mchakato huu hurudiwa kila baada ya miaka minne (4) kwa kuangazia tena maendeleo katika muktadha wa Utawala Bora. Nchi yenyewe au wanachama wengine wa APRM wanaweza kuamua kufanya tathmini kwa wakati mwingine wowote iwapo kuna hoja na haja ya kufanya hivyo, au kama nchi ingependa kufanya tathmini katika sekta za kimkakati zilizochaguliwa.

Kwa hiyo, Mpango huu ni endelevu, unaoamini kuwa siku moja Afrika itakuwa mfano wa Utawala Bora duniani hasa kwa kupata mifumo madhubuti wa kutatua changamoto za kiutawala.

Tujiunge sote kwa kutoa maoni katika kushiriki kuboresha utawala wa nchi yetu ya Tanzania na hatimaye hata kwa bara letu la Afrika.



*Wadau wa APRM wakijadili Ripoti ya Nchi.*


**Wasiliana nasi kupitia:**
**APRM Tanzania Sekretariati**
**Ghorofa ya 5, Jengo la JNICC**
**S.L.P. 8315**
**Simu Namba: +255 22 2129262/4/5/7**
**Nukushi: +255 22 2135029**


AFRICAN PEER REVIEW MECHANISM
APRM Tanzania

# APRM ni nini?


www.aprmtanzania.com
aprm@aprmtanzania.org